

# Waziri mkuu aagiza aliyekutwa na zana haramu za uvuvi akamatwe

**Na Mwandishi Maalum, Dodoma**

■ ■ WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa ameiagiza Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa (KUU) wa Mwanza imchukulie hatua za kisheria mfanyabiashara aliyekamatwa kwa makosa ya kujihusisha na biashara ya zana haramu za uvuvi.

"Yuko mfanyabiashara anaitwa Jeremiah Asam Omolo ambaye amekamatwa mara kadhaa kwa kukutwa na nyavu haramu. Wizara ilitoa specifications (aina ya nyavu) zinazoruhusiwa kutumika na KUU ya Mkoa ikasimamia lakini kuna maafisa wa Wizara waliingilia zoezi hilo mara tatu na akatozwa faini mara zote," amesema.

Waziri Mkuu ametoa agizo hilo jana wakati akizungumza na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mwanza kwenye kikao alichokifanya kwa njia ya video (video conference) kutokea ofisini kwake Mlimwa, jijini Dodoma.

Alisema kwa kuwa si mara yake ya kwanza kukamatwa, KUU ya Mkoa haina budi kuchukua hatua kali zaidi kwa sababu nia ya kutoa adhabu ni kumfanya mkosaji asirudie kosa lakini mfanyabiashara huyo amekuwa akilipa faini na kurudia makosa yaleyale.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella alisema katika kosa la kwanza, mfanyabiashara huyo alipatikana na marobota 66 ya nyavu haramu aina ya makila sawa na vipande 13,200 ambapo alitozwa faini ya sh. milioni 50.

Alisema katika tukio la pili, Aprili 3, mwaka huu, Omolo alikutwa na zana haramu za uvuvi aina ya makila vipande 6,964 na Timba vipande 179 na kutozwa faini ya sh. milioni 129.8.

"Katika tukio la tatu, Aprili 4, 2020 alipatikana na kosa la kumiliki zana haramu za uvuvi ambazo ni marobota 10 ya nyavu haramu aina ya makila sawa na vipande 300 na marobota 437 ya nyavu haramu aina ya Timba sawa na vipande 12,875 na kutozwa faini ya sh. milioni 300," alisema.

Alisema uongozi wa mkoa uliamua kuunda timu ya wataalamu inayojumuisha vyombo vya usalama ambayo itafuatilia na kuchunguza kwa undani mienendo ya mtuhumiwa huyo ikiwemo masuala la kikodi na ufanyaji wa biashara.

Mkuu huyo wa Mkoa alimweleza Waziri Mkuu kwamba timu hiyo iliyoundwa Aprili 9, mwaka huu, itapaswa kukamilisha kazi yake na kukabidhi taarifa yake, Jumatatu ijayo (Aprili 20, 2020).

**Wakati huo huo**, Waziri Mkuu alikemea mikusanyiko inayofanyika kwenye nyumba za ibada kwa kigezo cha kutaka watoto wasikae majumbani kwa vile hawaendi shuleni.

"Ninazo taarifa kwamba wameanzisha mfumo wa kupeleka watoto kwenye madarasa ya dini. Tumeruhusu ibada tu, na hizo ibada lazima ziangaliwe ziwe za muda mfupi kadri inavyowezekana. Tumesisitiza kwenye makanisa au misikiti ambako ibada zinafanyika, waumini wakae kwa kuachiana nafasi," alisema.

Alisema changamoto inajitokeza kwenye makanisa makubwa ambayo yana waumini karibu 3,000.

"Hayo sasa yatakuwa ni makongamano. Tunaaamini Maaskofu na Mufti wataliweka vizuri suala hili," amesema.

Alisema Serikali haitazuia biashara kwenye masoko, maduka au supermarkets isipokuwa amewataka wenye biashara hizo wahakikishe wanaweka ndoo za maji na sabuni ili wateja wanawe mikono kabla ya kuingia kupata huduma na wakati wanapotoka kupatiwa huduma hizo. Vilevile, amehimiza wananchi wazingatie kukaa umbali wa zaidi ya mita moja kutoka kwa mtu mwingine.

Kuhusu mikusanyiko mingine, Waziri Mkuu amesema watu wanapaswa wajizuie kwenda kuzagaa kwenye vituo vya mabasi na kama hawana shughuli za lazima za kufanya huko, basi wabakie majumbani kwao.

Scanned by CamScanner

# Kikosi maalumu chakamata shehena ya nyavu za uvuvi

**NA PETER BAIAN**

KIKOSI maalumu cha doria kudhibiti uvuvi haramu kanda ya Mwanza, kimefanikiwa kukamata robota 417 za nyavu haramu zenye thamani ya zaidi ya Sh bilioni 1.5, zikiwa zimefichwa kwenye nyumba moja eneo la Nyansaka Center wilayani Ilemela.

Kaimu Ofisa Mfawidhi wa Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi Kanda ya Mwanza, Jokomina Ntundu akitoa taarifa kwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongela alisema wamefanikiwa kukamata mzigo baada ya kuweka mtego.

Alisema nyavu hizo zilikamatwa kutokana na taarifa za siri kutoka kwa raia wema ambazo walifuatilia,kisha kufanikiwa kufika eneo la Nyansaka na kukuta mzigo huo, ukiwa umefichwa ndani ya nyumba iliyokuwa ya mpangaji aliyefahamika kwa jina moja la Juma.

"Baada ya mahojiano ya kina, ikiwemo kuomba mkataba ya mpangaji,ikaelezwa mzigo huo ni mali ya mfanyabiashara wa dhana za uvuvi jijini Mwanza, Jeremiah Assam maarufu Omolo mkazi wa Bwiru,"alisema.

Alisema mfanyabiashara Assam amefanikiwa kukamatwa na polisi wilayani Rorya na kusafirishwa hadi Mwanza ambapo anashikiriwa kituo kikuu cha Polisi Kati, huku robota zake za nyavu haramu zikiwa zinashikiriwa kituo cha polisi Nyakato.

"Hii ni mara ya pili Assam kukamatwa kwa tuhuma za kuingiza nyavu haramu ikiwa ni miezi miwili iliyopita alipokamatwa Machi, mwaka huu akiwa na nyavu haramu aina ya grinet 741, timber 178, kokolo moja na nyavu haramu tatu za dagaa ambazo thamani yake haijafahamika wakati akikamatwa na polisi wakati huo,"alisema.

Alisema amekuwa akifanya biashara haramu ya kuingiza nyavu haramu zikisubiri kusafirishwa kwenda maeneo mbalimbali ya kanda ya Ziwa Victoria kwa lengo la kuwauzia wavuvi kinyume na sheria za uvuvi.

Mongela aliagiza kuundwa kwa timu ya vyombo vya ulinzi na usalama kufatilia suala hilo, ikishirikiana na wataalamu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kuhakikisha hatua kali zinachukuliwa, ikiwemo kukomesha tabia ya wafanyabiashara kuendelea kuingiza nyavu haramu na kuishia kulipa faini ndogo ikiwa hailingani na madhala yatakayosababishwa na uvuvi haramu.

Mongela alisikitishwa na mfanyabiashara huyo aliyepigwa fani ya Sh milioni 120 alipofikishwa mahakamani mara ya kwanza alipokamatwa,ni vema wakaliangalia kwa upana hili la kutoza faini ndogo, ikiwa ni muda wa mwezi mmoja ambapo mwezi uliopita zaidi ya nyavu haramu 7,000 zilipatikana nyumbani kwake eneo la Bwiru jijini mwanza.

■ TABORA

Scanned by CamScanner

# Majaliwa aagiza aliyetozwa faini ya Sh470 milioni achukuliwe hatua

**Mwandishi Wetu**, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ameitaka Kamati ya Ulinzi na Usalama (KUU) mkoa wa Mwanza kumchukulia hatua za kisheria mfanyabiashara aliyekamatwa kwa kosa la kujihusisha na biashara ya zana haramu za uvuvi na kutozwa faini zaidi ya Sh470 milioni.

Amebainisha kuwa hatua pekee ambazo zilichukuliwa na Wizara ni kumtoza faini mfanyabiashara huyo kwa kumlipisha zaidi ya Sh470 milioni na kwamba si mara yake ya kwanza kukamatwa.,

Alisema kamati hiyo haina budi kuchukua hatua kali zaidi kwa sababu nia ya kutoa adhabu ni kumfanya mkosaji asirudie kosa lakini mfanyabiashara huyo amekuwa akilipa faini na kurudia makosa yaleyale.

"Lengo la Serikali siyo kutoza fedha peke yake, bali ni kudhibiti matumizi ya nyavu haramu nchini," alisisitiza.

Mtendaji mkuu huyo wa Serikali alitoa maagizo hayo jana wakati akizungumza na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mwanza kwenye kikao alichokifanya kwa njia ya video kutokea ofisini kwake Mlimwa, jijini Dodoma.

"Yuko mfanyabiashara anaitwa Jeremiah Asam Omolo amekamatwa mara kadhaa kwa kukutwa na nyavu haramu. Wizara ilitoa specifications (aina ya nyavu) zinazoruhusiwa kutumika na KUU ya Mkoa ikasimamia lakini kuna maafisa wa Wizara waliingilia zoezi hilo mara tatu na akatozwa faini mara zote."

"Mkuu wa Mkoa aliunda timu ya kuchunguza matukio haya. Hii ni timu ya Serikali na imeaminiwa kufanya kazi hii, na ina uwezo wa kuchukua hatua. Lazima KUU ya Mkoa isimamie na ichukue hatua. Hatuwezi kuwa na Wizara ambayo haiiamini KUU ya Mkoa," alisema.

Akifafanua makosa hayo, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella alisema katika kosa la kwanza, mfanyabiashara huyo alipatikana na marobota 66 ya nyavu haramu aina ya makila sawa na vipande 13,200 ambapo alitozwa faini ya Sh50 milioni.

Alisema katika tukio la pili, Aprili 3, mwaka huu, Omolo alikutwa na zana haramu za uvuvi aina ya makila vipande 6,964 na timba vipande 179 na kutozwa faini ya Sh129.8 milioni.

"Katika tukio la tatu, Aprili 4, 2020 alipatikana na kosa la kumiliki zana haramu za uvuvi ambazo ni marobota 10 ya nyavu haramu aina ya makila sawa na vipande 300 na marobota 437 ya nyavu haramu aina ya timba sawa na vipande 12,875 na kutozwa faini Sh300 milioni," alisema.

Alisema uongozi wa mkoa uliamua kuunda timu ya wataalamu inayojumuisha vyombo vya usalama ambayo itafuatilia na kuchunguza kwa undani mienendo ya mtuhumiwa huyo ikiwemo masuala la kikodi

**NUKUU**

"Yuko mfanyabiashara amekamatwa mara kadhaa kwa kukutwa na nyavu haramu. Wizara ilitoa specifications zinazoruhusiwa kutumika na KUU ya Mkoa ikasimamia lakini kuna maafisa wa Wizara waliingilia zoezi hilo mara tatu na akatozwa faini mara zote."

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa

Scanned by CamScanner